# LEARNING BY EAR 2011

## “The Promised Land- A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE THREE: “The Lucky and the Unlucky”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: FARAHANI AND SULE GET READY TO LEAVE**

- **Farahani (m, 25)**
- **Sule (m, 25)**

**SCENE TWO: CHIVASI HAS SUPPER WITH THE MARAGA FAMILY**

- **Linda (f, 20)**
- **Mr. Maraga (m, 60)**
- **Mrs. Maraga (f, 55)**
- **Chivasi (m, 22)**

**SCENE THREE: FARAHANI MEETS SULE AT A CYBER CAFE**

- **Farahani (m, 25)**
- **Sule (m, 25)**
- **Cyber café attendant ( f, 30)**

**SCENE FOUR: LINDA AND FLORENCE ON THE PLANE**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**
- **Pilot (m, 40)**
- **Small crowd talking in background (3-4 ppl)**

**INTRO:**

Hujambo na kwa mara nyingine karibu kwa makala hii ya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Hii ni makala ya tatu katika mfululizo wa mchezo huu wa redio **“Ardhi ya Ahadi” kuhusu “Waafrika wanaohamia barani Ulaya.”** Katika kipindi kilichotangulia, Linda anakabiliwa na changamoto wakati wa mahojiano ya kutafuta Viza katika ubalozi, lakini hatimaye anafaulu. Bila ya kutarajia, anakuta tayari Babake amemkatia tiketi ya kwenda Ulaya, na anapaswa kuondoka mwishoni mwa wiki. Mchumba wake Chivasi, bado hajaamini mchumba wake anasafiri Ulaya. Wanazungumza kwa njia ya simu na anakubali mualiko wa chakula cha jioni nyumbani kwa familia ya Linda. Kwa upande mwingine katika pwani ya Afrika Kaskazini, Farahani amevumbua mbinu ya kuwakwepa walinzi wa mpakani na kutorokea kisiri barani Ulaya. Sule anakubali kuandamana naye shingo upande. Nini kitakachotokea hii leo. Karibu uandamane nasi kwenye sehemu hii ya tatu **“Bahati na kutobahatika.”** Ni majira ya alfajiri huko Afrika kaskazini, jua limeanza kuchomoza. Farahani na Sule tayari wameamka na wameanza kujiandaa kwa safari yao.

**SCENE ONE: FARAHANI AND SULE GET READY TO LEAVE**

1. **SFX: MORNING ATMO, NORTH AFRICA (heard through the open**

**window): Birds outside, distant sounds of cars, and a muezzin calling.**

2. **FARAHANI:** **(in a rush)** Sule, fanya upesi! Msaidizi wetu anatusubiri kwenye gari hapo nje. Tumechelewa.

3. **SULE:** **(panicking)** Sizioni pesa zangu! Farahani, umenionea pochi yangu? Siwezi kumlipa mwenye gari ikiwa sitazipata pesa zangu.

4. **FARAHANI:** **(angrily)** Kwani pochi yako umeiweka wapi? Fanya upesi, Sule – Muda ni muhimu sana kwa hawa watu!

5. **SULE:** Nilikuwa nimeiweka mahali hapa…lakini sasa siioni. Utanilipia nauli? Kisha tukifika Ulaya nitakurejeshea pesa zako?

6. **FARAHANI:** Kwani unanichukuliaje mimi? Mjinga ehh? Nimesubiria siku hii kwa muda mrefu sana, na wewe hapa umeanza kughairi, kutaka kuniharibia mipango yangu yote!

7. **SFX: CAR HOOTING FROM DISTANCE SIGNALLING IMPATIENCE**

**8. SULE:** Sikiliza Farahani. Sisi ni marafiki, kama ndugu kabisa! Tafadhali nisaidie na kisha baada ya miezi michache nitaweza kukurejeshea pesa zako.

**9.**

**10. FARAHANI:** Sule, siwezi kukusaidia. Pesa nilizo nazo zanitosha mimi mwenyewe. Nauli imepanda sana hata kwa watu wanaoishi karibu na ufuoni! Tunahitajika kulipa kiasi cha Euro elfu moja kila mmoja, na hicho ndicho nilichonacho. Sahamani sana lakini naona nitakuacha.

**11. SFX: HOOTING GETS LOUDER AND LOUDER**

**12. SULE:** **(pleading)** Tafadhali, Farahani! Tafadhali zungumza na dereva - atatuelewa.

**13. FARAHANI:** Usiwe na wasi wasi, Sule. Wewe niombee safari njema. Nikifika Ulaya salama na mambo yakiniendea vizuri, nitafanya kila juhudi nikutumie pesa wewe pia uweze kusafiri.

**14. SFX: DOOR BEING OPENED**

**15. FARAHANI:** Kwaheri rafiki yangu Sule!

**16. SULE:** Farahani, tafadhali usiniache! Usiniache tafadhali!

**17. SFX: VAN ENGINE STARTS AND VAN DRIVES OFF SPEEDILY**

**18. FARAHANI:** **(shouting)** Subiri! Subiri!

**19. SULE:** **(bursts out laughing)** Hahahahaha!

**NARRATOR:** Sarakasi ya Farahani kufukuzana na gari lililojaa wahamahiaji haramu ilimfanya Sule kuangua kicheko. Farahani hakuwa akifukuzana na gari hilo tu bali pia ndoto yake ya kuhamia Ulaya. Je! atafanikiwa kujiunga na wenzake kwa safari hiyo. Endelea kusikiliza. Kwa upande mwingine, baadaye siku hiyo Chivasi anafika nyumbani kwa familia ya Maraga ambako amealikwa kwa chakula cha jioni kuagana na mchumba wake Linda anayejiandaa kusafiri Ulaya kwa masomo zaidi.

**SCENE TWO: CHIVASI HAS SUPPER WITH THE MARAGA FAMILY**

**20. SFX: DOG BARKING LOUDLY OUTSIDE (continues in background)**

**21. LINDA:** Huyo atakuwa ni Chivasi! Mbwa wetu hawampendi Chivasi.

**22. MR. MARAGA:** **(irritated)** Sio mbwa tu. Hata mamako pia hampendi Chivasi **(loud whisper).** Nadhani hajanisikia akiwa jikoni.

**23. LINDA:** Najua hivyo Baba. Hebu nimfungulie mlango.

**24. SFX: METAL DOOR BEING UNLOCKED**

**25. LINDA:** **(to dog)** Sporty, wacha, wacha!

**26. SFX: HAPPY DOG MAKING FAMILIAR FRIENDLY SOUNDS**

**27. CHIVASI:** **(jokes)** Samahani hapa ndio nyumbani kwa kina Linda Maraga?

**28. LINDA:** **(falls in with the joke)** Samahani, nadhani umekosea!

**29. CHIVASI:** Ni kweli dada, nadhani nimepotea bila ya yeye.

**30. LINDA:** **(giggles)** Nadhani pia amepotea bila ya kuwa nawe. **(changes tone)** Pita ndani wazazi wanakusubiri.

**31. SFX: METAL DOOR LOCKED**

**32. CHIVASI:** Habari za jioni Bw. Maraga.

**33. MR. MARAGA:** Njema Chivasi, karibu ndani **(calls out)** Mke wangu sasa idadi imekamilika.

**34. MRS. MARAGA:** Habari yako Chivasi! Sawa kabisa, sasa, kila mmoja anaweza kwenda kujipakulia chakula…. Tujisikie huru!

**35. SFX: PEOPLE SITTING DOWN**

**36. CHIVASI:** Mmm – chakula chanukia utamu!

**37. SFX: DINNER ATMO - PEOPLE SERVING THEMSELVES AND EATING**

**38. MR. MARAGA:** Ehhe, Chivasi, una mipango gani sasa?

**39. CHIVASI:** Kusema kweli sina mipango yoyote kwa hivi sasa. Kwani ndio mwanzo nimemaliza masomo yangu ya chuo kikuu.

**40. MRS. MARAGA:** Hutaki kuendelea na masomo yako?

**41. LINDA:** Tafadhali tunaweza kuzungumzia mambo mengine.

**42. CHIVASI:** **(a bit embarrassed)** Eeeh …kweli Bibi Maraga ningependa sana kuendelea na masomo yangu. Lakini mambo ni magumu sana kwangu. Wazazi wangu hawawezi kugharamia masomo yangu. Isitoshe kaka na dadangu zangu bado wanasoma. Kwa hivyo naonelea bora nipate kazi haraka iwezekanavyo ili niweze kuisaidia familia yangu.

**43. LINDA:** **(tries to change topic)** Tunaandamana na Chivasi kunisindikiza hadi uwanja wa ndege.

**44. MRS. MARAGA:** Oh, tunaandamana naye?

**45. CHIVASI:** **(caught off guard)** Ala naandamana na nyinyi?

**46. MR. MARAGA:** Ndiyo kwanini usiandamane nasi? Wewe ni mmoja wa familia hii Chivasi.

**47. CHIVASI:** Asante sana Bw. Maraga.

**48. LINDA:** Na punde nitakapomaliza masomo nitarudi hapa nyumbani, ningependa tuoane.

**(Silence)**

**NARRATOR:** Karibu Chivasi azimie kwa kusikia maneno hayo, sio tu kutoka kwa Linda mwenyewe bali wazazi wake pia. Na mshangao huo ukageuka kuwa faraja. Baada ya muda si mrefu ukawadia ule wakati wa Linda kuondoka. Katika uwanja wa ndege alikuwa amezungukwa na wazazi, jamaa na marafiki waliosoma pamoja, bila ya kusahau sabuni yake ya roho, Chivasi. Lakini kabla ya kumuaga Linda, hebu sasa tumgeukie Farahani tujue anavyoendelea baada ya kukosa safari ya kwenda Ulaya. Hajamuona Sule tangu siku walipoachana. Lakini huenda wakakutana kwenye kibanda cha Intaneti.

**SCENE THREE: FARAHANI MEETS SULE AT A CYBER CAFE**

**49. SFX: BUSY CYBER CAFE AMBIENCE**

**50. FARAHANI:** Tafadhali nisaidie na huduma ya Intaneti.

51. **ATTENDANT:** Utachukua muda gani?

52. **FARAHANI:** Kama nusu saa hivi.

53. **ATTENDANT:** Nenda Kompyuta namba tatu. Lakini lipa kwanza.

54. **SFX: COINS JINGLING WHEN COUNTED**

55. **SULE:** **(excited)** Farahani – Ni wewe? Samahani sana kwa -

56. **FARAHANI:** Sio sasa Sule. Tutazungumze baadaye tukimaliza.

57. **SULE:** Lakini isiwe umenikasirikia?

58. **FARAHANI:** Hata sijakasirika. Yote hayo ni mipango ya Mungu na hutokea kwa sababu! Na Mungu alikuwa amepanga wakati huo.

59. **SULE:** **(contemplating)** Ni kweli usemayo! Sikufikiria hayo. Labda nilikuwa kama Malaika wako?

60. **FARAHANI:** Malaika wa kunilinda. Hebu nisubiri hapa, narudi sasa hivi.

**NARRATOR:** Baadhi ya watu wamebahatika kuzaliwa katika familia tajiri, wengine familia zenye utajiri wa kadri kama Linda, na kunao wanaotoka

familia maskini kama Chivasi ,Farahani na Sule, ambao maisha yao ni magumu. Na matumaini yao ni kwenda kuishi kwenye maisha bora. Bila ya kupoteza muda zaidi Farahani anapanga safari nyingine. Na wakati huu anataka kuwatumia walanguzi wa watu. Watu wanaowasafirisha binadamu hadi Ulaya kinyume cha sheria . Wakati huo huo, Linda ameanza kufunga mkanda wa usalama kwenye ndege, akiwa na uoga mwingi. Karibu naye ni Florence, mwanamke wa umri wa miaka 30 hivi ambaye ameolewa na Mzungu. Florence anarejea Ulaya baada ya likizo kutembelea familia yake.

**SCENE FOUR: LINDA AND FLORENCE ON THE PLANE**

61. **SFX: ATMO INSIDE A COMMERCIAL AIRCRAFT CABIN (small crowd talking quietly in the background)**

**62. FLORENCE:** Hii ni mara yako ya kwanza kusafiri kwa ndege?

**63. LINDA:** Ndiyo. Hii ni mara yangu ya kwanza.

**64. FLORENCE:** Ohhh, usjali, utafurahia safari yenyewe. Naitwa Florence, lakini unaweza kuniita Flo.

**65. LINDA:** Naitwa Linda, Linda Maraga.

**66. FLORENCE:** **(cheerfully)** Nafurahi kufahamiana nawe Linda. Nadhani unaenda kumtembelea eee, mpenzi wako labda?

**67. LINDA:** Hapana, nimemuaga rafiki yangu sasa hivi kabla ya kuabiri ndege. Nasafiri Ulaya kwa masomo zaidi.

**68. FLORENCE:** Wow! Ni vizuri sana! **(changes tone)** Namaanisha masomo na sio mchumba wako! Najua huu ni wakati mgumu sana kwenu.

**69. LINDA:** Ndiyo. Lakini tutaoana pindi nitakapomaliza masomo yangu.

**70. FLORENCE:** Na utamaliza lini?

**71. LINDA:** Baada ya miaka mitatu. Nakwenda kusomea sheria za kimataifa.

**72. FLORENCE:** **(sceptically)** Miaka mitatu….hmm, sawa.

**73. LINDA:** Eee, Florence – Najua ndiyo mwanzo tumekutana, lakini eeehh nimependa sana rinda lako! Viatu, na mkufu wako wa dhahabu.

**74. FLORENCE:** Asante sana Linda. Unajua nini? Nimekupenda sana. Nitakupa nambari zangu za simu, ukiwa unahitaji msaada wangu au ungetaka kutembea nipigie simu wakati wowote. Sawa?

**75. SFX: gong (as for an announcement in a plane)**

**76. Pilot:** Karibuni katika safari hii nambari 7896. Rubani wa ndege hii ni mimi Smith. Ndege sasa iko tayari

kupaa kwa hivyo fungeni mikanda ya usalama na viti kubakia wima. Wafanyakazi wa ndege, tafadhali mketi katika nafasi zenu, tuko tayari kuondoka.

**77. SFX: PLANE GETTING READY FOR TAKE OFF**

**78. LINDA:** Asante sana Flo.

**79. FLORENCE:** Usijali furahia safari yako Linda.

**OUTRO:**

Na huku ndege inayombeba Linda ikipaa angani na kutokomea kwenye mawingu ya anga la Afrika kuelekea Ulaya, ndipo tunafika mwisho wa sehemu hii ya tatu kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio kuhusu Wa-Afrika wanaohamia barani Ulaya. Linda ameanza urafiki na Florence, lakini Je! mama huyu ni rafiki wa kweli? Nini kinachomsubiri Linda atakapowasili Ulaya? Na je! nyumbani, ni vipi mchumba wake Chivasi atakavyokabiliana na upweke na changamoto za maisha baada ya Linda kuondoka? Huko Afrika Kaskazini, Farahani ana mipango gani baada ya kushindwa kutorokea Ulaya na wahamiaji wengine haramu. Haya na mengine mengi, ungana nasi tena katika kipindi kitakachofuatia. Pia, unaweza kusikiliza tena kipindi hiki kupitia mtandao wetu dw-world.de/destinationeurope. Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.